

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA

20 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA – TAREHE 20 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya

Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

228. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati Shule za Msingi za zamani katika Wilaya za Ileje na Mbozi.

229. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara za mitaa ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa kwa kiwango cha lami kupitia miradi ya TACTIC.

230. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia miradi ya afya iliyoanzishwa kwa nguvu za Wananchi.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

231. MHESHIMIWA CAPT. ABBAS ALI HASSAN MWINYI (FUONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni kero gani za Muungano bado hazijapata ufumbuzi hadi sasa; na ni jitihada gani zinafanyika ili kero zilizosalia zipate ufumbuzi.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**232. MHESHIMIWA SANTIEL ERICK KIRUMBA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege katika Mkoa wa Shinyanga.

**233. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO
KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

● Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi barabara ya Handeni Kibirashi, Kondo hadi Singida kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MAJI:

**234. MHESHIMIWA SAMWEL XADAY HHAYUMA
(HANANG’):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Mradi wa Maji kutoka Ziwa Basotu kwa ajili ya Vijiji zaidi ya tisa utaanza kutekelezwa Wilayani Hanang’.

235. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji katika Kata ya Katuma ambayo ndiyo inatunza chanzo cha maji cha Mto Katuma.



WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:



236. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Uvinza.

**237. MHESHIMIWA JANEJELLY JAMES NTATE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Askari Polisi katika Kituo cha Polisi Kata ya Kilungule - Mbagala ili Wananchi wa Kata hiyo wapate huduma.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA
20 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**